**MKATABA WA BASEL KUHUSU UDHIBITI WA USAFIRISHAJI WA TAKA HATARISHI BAINA YA NCHI NA NCHI NA UTUPAJI WAKE.**

## 1. Utangulizi

Mkataba wa Basel unahusu udhibiti wa usafirishaji wa taka hatarishi baina ya nchi na nchi na utupaji wake. Mkataba huu ulianzishwa mwaka 1989 na ulianza kutekelezwa rasmi mwaka 1992. Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 1993.

Hadi sasa Mkataba una jumla ya nchi wanachama 191. Jumla ya aina 47 za taka hatarishi zinadhibitiwa na Mkataba wa Basel. Taka hatarishi ni pamoja na vyuma chakavu; betri chakavu; taka za plastiki; mafuta chakavu; mipira chakavu; mafuta machafu; taka za kielektroniki na taka zote zitokanazo na shughuli za migodi.

Mkataba wa Basel umeweka mfumo wa upashanaji habari na kupata ridhaa kutoka Mamlaka za usimamizi wa Mkataba wa Basel ya nchi zinazotegemea kupokea taka kabla ya kusafirishwa kwenda nchi hiyo (*Prior Informed Consent*).

## 2. Malengo ya Mkataba

i) Kupunguza uzalishaji wa taka hatarishi ili kulinda afya ya binadamu na mazingira;

ii) Kudhibiti usafirishaji wa taka hatarishi baina ya nchi na nchi;

iii) Kukuza ushirikiano wa pamoja baina ya nchi wanachama katika udhibiti wa taka hatarishi;

iv) Kuepuka baadhi ya nchi kufanya nchi zingine dampo la taka hatarishi wanazozalisha; na

v) Kuweka mifumo halali ya shughuli za taka hatarishi kwenye nchi husika ikiwa ni pamoja na ukusanyaji, uhifadhi na usafirishaji.

## 3. Ushiriki wa nchi katika Mikutano

i) Kushiriki kwenye mikutano ya kikanda ambapo nchi wanachama hupata nafasi ya kukutana, kujadili masuala muhimu ya Mkataba, kuainisha vipaumbele na changamoto za kikanda kwa ajili ya kuziwasilisha kwenye vikao vya nchi wanachama.

ii) Kushiriki kwenye mikutano ya nchi wanachama wa Mkataba wa Basel; ambapo nchi hupata nafasi ya kuchangia msimamo wa masuala ya usimamizi wa taka hatarishi kulingana na agenda zinazobainishwa.

iii) Kushiriki warsha kuhusu usimamizi na udhibiti wa taka hatarishi zinazoratibiwa na Sekretarieti ya Mkataba, vituo vya Kikanda na wadau wengine.

### 4. Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba

i) Kufanya Tathmini ya uwezo wa Kitaasisi katika kusimamia taka za plastiki zinazovuka mipaka; na

ii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Taka Hatarishi za Mwaka 2021 na Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2021 kwa kumshauri Waziri mwenye Dhamana kutoa vibali.

### 5. Fursa zilizotokana na mkataba

i) Upatikanaji wa rasilimali fedha kupitia Miradi inayotekelezwa nchini;

ii) Misaada ya kitaalamu kupitia warsha na mafunzo yanayoandaliwa na Sekretariet ya Mkataba

### 6. Changamoto za utekelezaji wa mkataba

i) Baadhi ya nchi kuchelewa ama kutokutoa kabisa idhini ya kupokea taka zinazosafirishwa nje ya nchi;

ii) Baadhi ya nchi kuingiza taka nchini bila kufuata taratibu na matakwa ya nchi;

iii) Baadhi ya wafanyabiashara nchini kufanya shughuli za taka hatarishi bila ya kuwa na vibali vilivyotolewa na Waziri; na

iv) Baadhi ya wadau wasiokuwa waaminifu kuhujumu miundombinu ya nchi kwa ajili ya biashara ya vyuma chakavu.